# THE CURVE EVALUATION TEST
## DARASA LA NANE - MWAKA 2022
**(GOLD)**
# KISWAHILI
***Muda: Saa 1 Dakika 40***

***Chagua neno lifaalo kujazia mianya iliyoachwa kutoka swali la 1 - 15***

Binadamu yeyote mustaarabu ____1____ mwenziwe ____2____ matatizo, inafaa ____3____ na ikiwezekana ____4____. Hata hivyo ____5____ wetu hatufanyi ____6____. ____7____ yake wenzetu ____8____ wanapopatwa na janga. Wale wanaowasaidia wenzao, ni watu wenye utu. Binadamu anastahili kuwa na moyo wa kuwasaidia ____9____, si vyema hata kidogo kutokuwa na moyo wa kusaidia. Kumbuka kuwa akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** alimwona | **B.** atamwona | **C.** anamwona | **D.** anapomwona |
| **2.** | **A.** kwa | **B.** ndani | **C.** katika | **D.** wa |
| **3.** | **A.** amsikitikie | **B.** amsikitikie huruma | **C.** asimwone huruma | **D.** amtoe |
| **4.** | **A.** amuibie | **B.** amcheke | **C.** ambeze | **D.** amuinue |
| **5.** | **A.** wengine | **B.** kati | **C.** miongoni | **D.** wengi |
| **6.** | **A.** mengi | **B.** hivyo | **C.** hicho | **D.** yayo |
| **7.** | **A.** Bali | **B.** Badala | **C.** Kinyume | **D.** Baada |
| **8.** | **A.** ninawacheka | **B.** mnawacheka | **C.** mnacheka | **D.** tunawacheka |
| **9.** | **A.** kwenyewe | **B.** wengine | **C.** nyingine | **D.** wengine |

Ni jukumu la kila mzazi ____10____ watoto wake. ____11____ yafaao ni kushughulikia mtoto kwa njia ____12____ ile. Lazima ____13____ kwamba mtoto anafundishwa kuwa na ____14____ kwa lolote ambalo ____15____. Heshima na adabu ni muhimu sana katika maisha ya mtoto.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | **A.** kuwalea | **B.** kulewa | **C.** kuwalelea | **D.** kumlea |
| **11.** | **A.** Malezi | **B.** Mlezi | **C.** Walezi | **D.** Ulezi |
| **12.** | **A.** kote | **B.** yoyote | **C.** zote | **D.** yote |
| **13.** | **A.** ihakikishiwe | **B.** hakika | **C.** ihakikishwe | **D.** ihakikishue |
| **14.** | **A.** ramani | **B.** adhabu | **C.** adimu | **D.** nidhamu |
| **15.** | **A.** hulifanya | **B.** hufanya | **C.** analofanya | **D.** afanyako |


***Kuanzia nambari 16-30, jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

***Kanusha sentensi hii***

**16.** Baba amekuja
A. Akina baba wanakuja
B. Akina baba hawajaja
C. Baba hajaja
D. Mama ameenda

**17.** Andika katika udogo
**Mti huu una matunda matamu**
A. Jiti hili lina majitunda matamu
B. Vijiti hivi vina vijitunda vitamu
C. Kikimti hiki kina vitunda vitamu
D. Kijiti hiki kina vijitunda vitamu

**18.** Taja jina la umbo hili



A. mche mstatili  B. mche mraba
C. mraba  D. mshazari

19. Tumia kiashiria takriri sahihi. Vikombe __________ vilianguka hapa
A. hivyo hivyo B. vivi hivi
C. hivyo hivi D. hivi vivi

20. Vidudu vidogo ambavyo huishi kwa wingi kwenye mwili wa kuku na ndege wengine na kuwaletea ugonjwa huitwa:
A. utitiri B. chawa
C. viroboto D. funza

21. Mtoto aliimbiwa wimbo mpaka akalala. Neno lililopigwa mstari liko katika kauli gani?
A. kutendewa B. kutendeka
C. kutendeana D. kutendwa

22. Maelezo yapi kati ya haya ni sahihi
A. Mlamu - Ndugu wa kiume wa mume au mkeo
B. Mcheja - jina la heshima waitanalo mume na wazazi wa mke
C. Mkoi - mwana wa kilembwe
D. Bavyaa - babake mume

23. Kuku hukaa kwenye____ilhali konokono hukaa kwenye______.
A. Kizimba/Kombe
B. Kiota/Kombe
C. Kizimba/Tundu
D. Tundu/Pango

24. *"Chini ya, Kando ya,Karibu na".* Vifungu hivi vya maneno viko katika kipengele kipi cha lugha?
A. Vimilikishi B. Viashiria
C. Vielezi D. Vihusishi

25. Chagua sentensi yenye **"KI"** ya masharti
A. Nilimkuta akipika chakula
B. Kitoto kigonjwa kimetibiwa
C. Ukipanda utavuna
D. Nilikipata kioo changu.

26. Andika sentensi hii bila "amba"
Jumba ambalo linajengwa.
A. Jumba linajengwa.
B. Jumba lijengwalo.
C. Jumba linajengwalo.
D. Jumba lilijengwa.

27. Andika wingi wa sentensi ifuatayo
**Seremala alipiga ubao wote randa.**
A. Seremala walipiga ubao wote randa.
B. Maseremala walipiga ubao wote randa.
C. Seremala walipiga mbao yote randa.
D. Maseremala walipiga mbao zote randa.

28. Ni ipi isiyo maana ya neno kata?
A. Kitambaa cha kuchukulia mizigo kichwani.
B. Ondoa sehemu ya kitu.
C. Sema au onyesha hali ya kutokubaliana
D. Mtaa.

29. Nyambua kitenzi **ezeka** katika hali ya kutendua
A. Ezekea B. Ezekua
C. Ezekwa D. Ezua

30. **Kamilisha methali hii**
Mali ya bahili__________
A. huliwa na wadudu
B. huliwa na utitiri
C. hunasa japo nyingi
D. nzi kufa juu yake si haramu

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40***

Hapo zamani kabla ya pesa kugunduliwa watu walifanya biashara kwa kubadilishana vitu. Kwa mfano mfugaji alipotaka apate mahindi toka kwa mkulima, alimpelekea ng'ombe ndipo mkulima ampatie mahindi yanayolingana na thamani ya ngo'mbe huyo.

Biashara ilikuwa ngumu sana kwa sababu pesa hazikutumika. Ilikuwa vigumu watu kubadilisha vitu kwa mfano mhunzi anaweza kuwa na visu vyake alivyofua na anahitaji mchele wa mkulima. Mkulima naye anaweza asiwe na haja ya visu lakini anahitaji chumvi hiyo na kupewa mchele. Wakati mwingine ilitokea kwamba hakuna mtengenezaji wa chumvi ambaye anahitaji visu lakini wapo waliohitaji vyungu vya kuwekea awape visu nao wampe vyungu, kisha apeleke vyungu kwa mtengenezaji chumvi ambaye atampatia chumvi. Akishapata chumvi hiyo ndipo huipeleka kwa mkulima akapewe mchele.

Ugunduzi wa pesa umefanya biashara iwe rahisi. Pesa ni kiungo cha kubadilishana bidhaa. Kazi kuu ya pesa ni kupima thamani ya vitu. Vile vile pesa hutunza thamani ya vitu. Mtu akipata pesa kwa kuuza vitu vyake anaweza kuzitumia kununua vitu vya aina nyingine wakati wowote. Sio lazima azitumie siku ile ile. Hivyo mhunzi hana haja ya kutafuta mtu wa kubadilishana naye visu vyake ndipo apate mahindi. Mtu yeyote anayetaka visu atakwenda na pesa kwa mhunzi kununua. Mhunzi akishauza visu vyake hutumia pesa anazopata kwenda kwa mkulima kununua mchele.

Pesa za zamani hazikufanana na za siku hizi. Watu wa sehemu mbalimbali duniani walitumia vitu tofauti kama pesa. Simbi za makomba ya baharini zilitumika kama pesa, shanga,pembe za ndovu,mawe ya rangi nzuri kama yakuti na lulu,vipande vya dhahabu, fedha, shaba na hata kucha za wanyama kama simba na chui. Aina ya pesa ambayo imeendelea kutumika toka zamani mpaka sasa ni dhahabu na fedha lakini hizi pia siku hizi hazitumiki hadharani, zinatunzwa kwenye benki.

**31.** Kutokana na ufahamu:
A. Pesa zilígunduliwa zamani za kale.
B. Zamani watu walikuwa wanabadilishana vitu.
C. Watu hawakuwa wakifanya biashara zamani
D. Ilikuwa vigumu sana watu kuwasiliana.

**32.** Mfugaji alipotaka kupata mahindi alifanya nini?
A. Alienda kununua mahindi kutoka kwa mkulima.
B. Alienda kwa mhunzi kubadilishana na ng'ombe
C. Alienda kwa mtegeneza chumvi kupewa pesa.
D. Alienda kubadilisha ng'ombe na mahindi.

**33.** Kwa nini biashara zamani ilikuwa ngumu?
A. Pesa hazikuwa zimegunduliwa.
B. Watu hawakuwa na vitu vingi vya kubadilishana
C. Si watu wengi walifurahia kutumia pesa
D. Watu hawakuwa wakielewana.

**34.** Ni jambo gani limefanya biashara iwe rahisi?
A. Watu kuelewana na kubadilishana bidhaa.
B. Wahunzi kutengeneza vitu vingi.
C. Ugunduzi wa pesa.
D. Watu kukubali kubadilisha na bidhaa zao.

**35.** Aina ya pesa inayoendelea kutumika toka zamani mpaka sasa ni
A. shanga B. dhahabu
C. simbi D. noti

**36.** Mtu anapopata pesa:
A. Si lazima azitumie siku ile ile amezipata.
B. Inambidi aende kwa mhunzi.
C. Ni lazima anunue kitu na hizo pesa.
D. Hawezi kuzitumia kwa njia nyingine.

**37.** Siku hizi mhunzi akitaka mchele:
A. Ni lazima abadilishe mchele na visu
B. Ni lazima kwanza abadilishe visu na chumvi.
C. Anafaa kwanza aende kwa benki
D. Anaweza kuuza visu na akanunue chumvi.

**38.** Mtu anayetaka visu siku hizi hufanya nini?
A. Huweza kuzipata kutoka kwenye benki
B. Huenda na ng'ombe abadilishiwe.
C. Huchukua pesa na kwenda kununua visu.
D. Huenda na visu vya kubadilishana na mhunzi.

**39.** Kazi kuu ya pesa ni:
A. Kufanya watu wote washiriki kwenye biashara.
B. Kumfanya mtu awe tajiri
C. Kumfanya mtu aende kwa benki.
D. Kupima thamani ya vitu.

**40.** Kichwa mwafaka kwa ufahamu huu ni
A. Jinsi mhunzi anaweza kupata visu
B. Mtengeneza chumvi na mhunzi
C. Matumizi ya pesa katika biashara.
D. Ugunduzi wa kubadilishana vitu.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50</u>***

Uamuzi uliofanywa na serikali wa kuhimiza watoto wote warudi shuleni ni jambo mwafaka sana. Watoto walifurika furi furi shuleni kusajiliwa. Wale waliokuwa wakirandaranda mitaani walifuatilizwa hima hima na kupelekwa shule. Waliokuwa wakubwa ki umri walipelekwa kwenye shule za ufundi.

Kwa miaka mingi, <u>baadhi ya wazazi walikuwa wameshindwa kuwasomesha wana wao</u>. Hii ni kutokana na umaskini uliokithiri mipaka. Hali hiyo ilichangia huzuni kuu miongoni mwa familia. Pengo la waliosoma lilizidi kuwa pana kielimu na kiuchumi. Uadui ukaingilia jamii pamoja na ujambazi na ukaidi.

Sasa watu wote waliokwepa haki sawa ya kusoma watakinaisha kiu chao. Pia mengi ya matatizo yatapungua. Si kweli kuwa tajiri ni mwerevu kuliko mkata. Kila mwanajamii akipewa nafasi ya kusoma kwa bidii atafua dafu maishani.

Vijana watakaofuzu katika shule za kiufundi wataweza kuajiriwa katika sekta mbalimbali. Mwishowe wakipata mtaji watajiendeleza kwa kuanzisha miradi midogomidogo ya kujitegemea. Hali kama hii katika shule ikienea kote nchini viwanda vidogovidogo vitaanzishwa na ajira itapatikana.

Hivyo njia mojawapo kuu ya kuinua uchumi na kuzalisha nafasi nyingi za kazi ni kuiendeleza elimu. Kitaaluma hawa vijana wataweza kuwa daktari, wasanii, waalimu na kazi zingine nyingi. Kisomo ni kitamu hakifai kutiliwa nanga.

41. Uamuzi uliofanywa na serikali
A. ulisababisha kufurika kwa watoto shuleni na kuleta umaskini.
B. ulisababisha kuchipuka kwa vyuo vya ufundi na kuondoa umaskini.
C. ulisababisha kuongezeka kwa watoto shuleni na kupata nafasi ya kujiendeleza.
D. ulisababisha kupungua kwa umaskini na kuwapa watoto nafasi ya kujiendeleza

42. *"........baadhi ya wazazi walikuwa wameshindwa kuwasomesha watoto wao..."* Chagua methali inayoweza kueleza hali hii.
A. Maskini kupata ni mwenye nguvu kupenda
B. Dua la mnyonge haliendi joshi.
C. Ng'ombe wa maskini hazai mapacha.
D. Maskini halali mchana.

43. Ukosefu wa elimu husababisha
A. Umaskini,uadui,huzuni na ujambazi
B. Wivu,ujambazi,kukosa kiu ya kusoma na uadui
C. Utajiri,ukosefu wa kazi,huzuni na ujambazi
D. Ujambazi,wivu,utajiri na kiu ya kusoma

44. Kulingana na kifungu hiki, pengo kubwa la kiuchumi limesababishwa na
A. watoto kutopata kisomo kwa sababu ya umaskini.
B. uadui na ujambazi uliokumba jamii maskini.
C. wazazi kushindwa kupambana na umaskini
D. watoto kutopelekwa shule za ufundi kwa sababu ya umaskini

45. Ni kweli kuwa watu wote wakipewa nafasi sawa________
A. Watoto wote wapendao kusoma watakuwa tajiri
B. Watoto wote wapendao kusoma watapata kisomo.
C. Watoto wa maskini watakuwa werevu.
D. Watoto wote wa matajiri na maskini watakuwa sawa.

46. Vijana wote wakipata mali________
A. wataanzisha miradi ya kiufundi.
B. wataweza hata kuwa wataalamu
C. wataanzisha shughuli za kujikimu.
D. watakitilia kisomo chao makini

47. Kisomo hakifai kutiliwa nanga kwa sababu
A. Watu watakuwa wataalamu.
B. Kina manufaa mengi
C. Shule zitapanuka
D. Serikali itakigharamia

48. Maana ya <u>kusajiliwa</u> ni________
A. kunufaisha
B. kurekebisha
C. kuandikishwa
D. kufundishwa

49. *Watakinaisha kiu chao,* ina maana ya ________
A. watapunguza tamaa zao
B. wataacha hofu yao
C. watafurahia hali yao.
D. watatosheleza hamu yao.

50. Kichwa kinachofaa zaidi kwa taarifa hii ni
A. Ukarimu wa serikali
B. Kupunguza ujinga
C. Masomo ya kiufundi
D. Serikali kupanua masomo